

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) leo tarehe 30 Novemba, 2020 atawaapisha Wabunge wawili walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Tukio hilo litafanyika katika Viwanja vya Bunge Jijini Dodoma saa 10:00 jioni.

Wabunge hao walioteuliwa tarehe 29 Novemba, 2020 ni Bwana Humphrey Polepole ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC), Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Bi Riziki Said Lulida aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Bunge la 11 kupitia Chama cha Wananchi CUF.

Mheshimiwa Spika atawaapisha Wabunge hao kwa kuzingatia Kanuni ya 30 (2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kanuni hiyo inaeleza kuwa endapo Mbunge atachaguliwa au kuteuliwa katika kipindi ambacho hakuna Mkutano wa Bunge unaoendelea, Spika atamwapisha katika eneo atakalolipanga na atatoa taarifa kwenye Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge unaofuata.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,

Ofisi ya Bunge,

**DODOMA.**

**30 Novemba, 2020**